

BARAZA LA FAMASI



UTARATIBU WA UHUISHAJI WA TAARIFA ZA WANATAALUMA WALIOPO KWENYE REJESTA

UTANGULIZI

1. **DHUMUNI:** Kutekeleza takwa la Kifungu Na. 22, 26 na 30 vya Sheria ya famasi ya mwaka 2011 (*The Pharmacy Act 2011*) Sura 311.
2. **WAHUSIKA:** Wafamasia, Fundi Dawa Sanifu na Fundi Dawa Wasaidizi.
3. **MFUMO WA UHUISHAJI:** Mfumo wa kieletroniki utamtaka mwanataaluma kuwasilisha taarifa zake za sasa kwa Msajili kwa mujibu wa Sheria.

LENGO LA UTARATIBU

1. **BARAZA:** Kurahisisha utendaji kazi nautoaji wa huduma kwa haraka.
2. **WANATALUUMA:** Kupunguza gharama na upotevu wa muda kwa ajili ya ufuwatiliaji wa taratibu, uwasilishaji wa taarifa na upatikanaji wa leseni.

UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA MWANATAALUMA KWENYE REJESTA

- a) **FOMU:** Jaza fomu inayopatikana kwenye tovuti www.pc.go.tz kisha bonyeza huduma za kimtandao (*Online Services menu*) kisha bonyeza *Retention Application*; (*Sign up*)
<http://196.45.42.57/pcmis.data/view/modules/registration/pharmacist-signup.php>
Sign in: <http://196.45.42.57/pcmis.data/>
- b) **ADA:** Lipa ada ya kushikilia jina kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Wanataaluma ya mwaka 2005 na Kanuni za Ada na Tozo ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2012 kama ifuatavyo:-

| | |
|---------------------------|---------------|
| Mfamasia | TZS 165,000/- |
| Fundi dawa sanifu | TZS 66,000/- |
| Fundi dawa msaidizi | TZS 44,000/- |
- c) **MUDA WA MALIPO:** Mwisho wa kulipia ada ni tarehe 30/01/2021, baada ya hapo utalazimika kulipa pamoja na faini ya asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango alichotakiwa kulipia.

MAMBO YA KUZINGATIWA WAKATI WA KUHUISHA TAARIFA ZAKO KWENYE REJESTA

- a) **JINA:** ni kwa mujibu wa cheti cha usajili (Registration, Enrollment, or Enlisting certificate);
- b) **NAMBA YA USAJILI** (Registration, Enrollment or Enlisting Number): imetoholewa na kutoa Personal Identification Number (PIN) kwa mfano ifuatayo:-

| S/N | KADA | NAMBA YA USAJILI | KEY CODE | PIN (PERSONAL IDENTIFICATION NUMBER) |
|-----|---------------------|------------------|----------|--------------------------------------|
| 1. | Mfamasia | 754 | 01 | 00000 mfano 0100754 |
| 2. | Fundi Dawa Sanifu | 1010 | 04 | 00000 mfano 0401010, |
| 3. | Fundi Dawa Msaidizi | 24 | 05 | 00000 mfano 0500024 |

Hata hivyo kwa wale ambao wana leseni tayari PIN zimeanishwa kwenye vitambulisho hivyo.

- c) **PICHA:** wasilisha (*upload*) nakala laini ya picha ya uso (*passport size*) yenye *Blue Background* zingatia vipimo *width 350px height 350px*.
- d) **MAFUNZO ENDELEVU** (*additional qualification*): wasilisha nakala laini ya vyeti vya mafunzo endelevu aidha kozi za muda mrefu na muda mfupi;
- e) **LESENI YA UTENDAJI KAZI:**
 - i. Jaza tarehe ya kutolewa (*Issued*) kwa leseni ya mwisho
 - ii. Leseni hutumika kwa muda wa miaka miatu (03). Leseni iliyotolewa (*issued*) 2019 itatumika hadi 2021 na iliyotolewa 2020 itatumika hadi 2022.
- f) **MALIPO:**
 - (i) *Control Number* itapatikana kwenye mfumo (*automatically*) wakati wa kuwasilishwa maombi sehemu ya *Bill Creation* na kutumwa kwenye namba yako ya simu.
 - (ii) *Control Number* hii itakuwa na uhai ambao utakoma matumizi tarehe 31/01/2021.
 - (iii) Tembelea akaunti yako sehemu ya *Bill Creation* kuweza kupata namba mpya ya malipo baada ya tarehe 31/01/2021 ambayo itaambatana na faini ya 25%:
- g) **USER MANUAL:** Kabla ya kuanza kujaza taarifa zako kwenye *Pharmacy Council Online Retention Application System (PCORAS)* hakikisha unasoma *User Manual* <https://www.pc.go.tz/files/PharmaceuticalPresonnelRetentionUserManual.pdf>

Imetolewa na:

Msajili, Baraza la Famasi

S.L.P. 1277, Dodoma

Simu: 0756710791/0800110015

Barua pepe: info@pc.go.tz /registration@pc.go.tz